

**MAJIBU YA HOJA ZA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI, OKTOBA – DISEMBA, 2016/2017**

NA	MAELEZO YA HOJA	USHAURI WA MKAGUZI	MAJIBU YA OFISI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA MKAGUZI BAADA YA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI
1	<p><b>Kutokuwepo kwa Rejista ya Kutunzia Hundi Zilizokataliwa na Benki.</b></p> <p>Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa rejista ya kutunzia kumbukumbu za hundi ambazo zimerudishwa kutoka benki bila kufanyiwa malipo au kuingizwa kwenye akaunti kutokana na sababu mbali mbali. Hii ni kinyume na Mwongozo wa fedha za serikali za mitaa ya mwaka 2009 agizo Na.5 (11) ambalo linataka kuwepo na rejista maalum ya kutunzia kumbukumbu za hundi zote zilizokataliwa au kutofanyiwa malipo na benki.</p>	<p>Menejimenti inashauriwa kuandaa na kuitunza ipasavyo rejista ya kumbukumbu za hundi mbalimbali ili kuboresha udhibiti wa malipo na mapokezi ya hundi.</p>	<p>Rejista inaandaliwa kwa sasa na kuingizwa taarifa zote muhimu na itakapokamilika italetwa kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p>Rejista iandaliwe na kukabidhiwa Mkaguzi kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p>Rejista tayari imeshaandaliwa na imeletwa kwa ajili ya ukaguzi. (Hoja hii imefungwa)</p>
2.	<p><b>Kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kila mwezi.</b></p> <p>Ukaguzi uliofanyika umebaini kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa baadhi ya akaunti.</p> <p>Aidha kutotayarishwa kwa taarifa za usuluhishi inakuwa ni vigumu kujua bakaa ya fedha kwa kila mwezi na usalama wake benki. Hii ni</p>	<p>Idara ya fedha inatakiwa kuandaa taarifa za usuluhishi wa kibenki kila mwezi na kwa kila akaunti</p>	<p>HOJA HII HAIKUJIBIWA</p>	<p>Wahusika wajulikane na hoja hii ijibiwe kabla ya tarehe 24/02/2017</p>	<p>Akaunti mbili ambazo ni Akaunti ya <b>Mishahara (PE)</b> na Akaunti ya <b>Mapato ya ndani</b> bado hazijafanyiwa Usuluhishi wa kibenki hadi tarehe 27/02/2017</p>

NA	MAELEZO YA HOJA	USHAURI WA MKAGUZI	MAJIBU YA OFISI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA MKAGUZI BAADA YA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI
	kinyume na mwongozo wa fedha za serikali za mitaa wa mwaka 2009 agizo la 29(2) na Mwongozo wa uhasibu kifungu cha 7.1 ambavyo vinamtaka mweka hazina kuhakikisha kuwa taarifa za usuluhishi wa kibenki zinaandaliwa kila mwezi kwa akaunti zote.				
3	<p><b>Kiasi cha Tshs 105,376,388 hazijapelekwa Benki kwenye akaunti ya Amana.</b></p> <p>Baada ya Ukaguzi wa usuluhishi wa benki tumebaini hundi zenye kiasi cha Tshs 105,376,388 zilizotakiwa kuingizwa kwenye akaunti ya amana. Hadi sasa fedha hizo bado hazikuingizwa kwenye akaunti husika. Hii ni kwenda kinyume na Mwongozo wa uhasibu wa mwaka 2009 kifungu cha 7.1 na Mwongozo wa fedha wa 2009 Agizo la 29(2) ambavyo vinaelekeza kutayarishwa kwa usuluhishi wa benki.</p>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Idara ya fedha inatakiwa kuandaa taarifa ya usuluhishi wa benki kila mwezi.</li> <li>2. Miamala yote iliyopo kwenye taarifa za usuluhishi wa benki inatakiwa ifanyiwe marekebisho.</li> </ol>	Hakuna majibu kutoka idara ya fedha mpaka tarehe ya 18.01.2017	Apatiwe Mhasibu wa kushughulikia kwa barua ya uteuzi na majukumu na barua iwasilishwe kwenye kikao cha kamati ya ukaguzi kijacho.	Idara inajipanga katika kugawana majukumu kwani aliyekuwa mhasibu wa akaunti hii amehamishwa kwenda ofisi ya Katibu Tawala.
4.	<p><b>Malipo yenye Thamani ya Tshs 28,269,575 Hayakuwa na Viambatanisho vya Kujitosheleza.</b></p>	Mhasibu anaehusika na malipo ahakikishe kuwa malipo yanafanyika kwa nyaraka zile tu amabazo zina viambata tosholezi.	Viambata vyote vimepatikana na vitaletwa kwa ajili ya uhakiki kwa sababu	Mhasibu apewe muda kidogo awasilishe viambata tajwa kabla ya tarehe 24/02/2017	Viambata vimeletwa na kuhakikiwa, hivyo hoja hii IMEFUNGWA

NA	MAELEZO YA HOJA	USHAURI WA MKAGUZI	MAJIBU YA OFISI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA MKAGUZI BAADA YA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI
	Tulibaini kuwa malipo yenye thamani ya Tshs 28,269,575 ya mradi wa Kuboresha Elimu Tanzania hayakuwa na viambatanisho vya kujitosheleza. Hii ni kinyume na Mwongozo wa uhasibu wa mwaka 2009 kifungu 2.4 ambacho kinaelekeza mambo ya kuzingatia wakati wa malipo. Kitengo cha ukaguzi wa awali (pre audit) hakikubainisha mapungufu hayo kwenye hati za malipo.		zilihifadhiwa sehemu nyingine kimakosa		
5.	<p><b>Matumizi Yenye Thamani Ya Tshs 3,622,000 ya Mradi wa Kuboresha Elimu Tanzania yalikuwa na Makosa Mbali Mbali.</b></p> <p>Ukaguzi umebaini kuwa, baadhi ya hati za malipo zilikuwa na kasoro kama kutoidhinishwa kwa hati hizo. Hii ni kinyume na Mwongozo wa fedha wa mwaka 2009 kifungu namba 8(2) C ambacho kinamtaka mweka hazina kutunza ipatsavyo nyaraka zote zilizo chini yake. Kitengo cha ukaguzi wa awali (pre audit) hakikubainisha mapungufu hayo kwenye hati za malipo..</p>	Kitengo cha ukaguzi wa awali lazima kifanye ukaguzi wa awali wa hati zote za malipo kabla ya malipo yoyote kufanyika.	Mapungufu na kasoro zote zimerekebishwa na hati hizo za malipo zitaletwa kwa ajili ya uhakiki	Isijirudie, Mkaguzi wa ndani afuatilie kuona kuwa mapungufu hayo hayajirudii tena.	Hati ya malipo imeshaidhinishwa, Hivyo HOJA HII IMEFUNGWA.
6.	<b>Fedha Kiasi cha Tshs 820,000 toka Mpango</b>	Mratibu wa mpango wa	Nyaraka zote muhimu	Ziletwe nyaraka halisi zinazoonesha	Wahusika wamesema kulikuwa na umuhimu

NA	MAELEZO YA HOJA	USHAURI WA MKAGUZI	MAJIBU YA OFISI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA MKAGUZI BAADA YA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI
	<p><b>wa Kuboresha Elimu zilitumika kinyume na Bajeti ya Mwaka</b></p> <p>TShs 820,000 kutoka katika mradi wa Equip zilitumika kinyume na bajeti ya mwaka iliyopangwa. ambapo Tshs 670,000 zilitumika kama posho na 150,000 zilitumika kukodi ukumbi. Tulibaini kuwa shughuli hizi zilipangwa kufanyika kwa siku nne lakini zikafanyika kwa siku sita. Hii ni kinyume na bajeti iliyopitishwa ya mpango husika wa EQUIP.</p>	<p>kuboresha elimu ahakikishe kuwa shughuli zilizo pangwa kufanyika ndizo zinazotekelezwa.</p>	<p>zimepatika kwa sasa zipo tayari kwa ajili ya uhakiki kwa sababu zilihifadhiwa kwenye mabechi mengine.</p>	<p>ongezeko la siku hizo, kabla ya tarehe 24/02/2017</p>	<p>mkubwa wa kuongeza siku hiyo ili kukamilisha mafunzo hayo kwani kutokamilika kwa mafunzo hayo kungekuwa na madhara Zaidi. Hivyo HOJA HII IMEFUNGWA.</p>
7	<p><b>Upungufu wa Kiasi cha Matumizi Kwa Tshs. 6,704,000 Kwenye Taarifa ya Matumizi ya Mwaka 2016 ya Mradi wa Kuboresha Elimu.</b></p> <p>Ukaguzi wa matumizi ya mpango wa kuboresha elimu ulibaini kuwepo kwa matumizi yenye jumla ya Tshs 309,999,545. Aidha taarifa iliyoandaliwa na Mratibu wa mpango ilionesha matumizi ya Tshs 303,245,545. Kuna tofauti ya Tshs 6,704,000 ambayo haikutolewa maelezo. Hii ni kinyume</p>	<p>Taarifa ya mapato na matumizi ya mradi wa EQUIP ifanyiwe marekebisho kulingana na mapungufu yaliyonekana na marekebisho yaletwe ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki</p>	<p>Taarifa ya mapato na matumizi ya EQUIP kuishia Juni, 2016 ni sahihi kama ilivyoandaliwa na haina mapungufu yoyote uthibitisho</p>	<p>Nyaraka hizo zipelekwe kwa mkaguzi mkuu wa ndani kwa ajili ya uhakiki kabla ya tarehe 24/02/2017</p>	<p>Nyaraka zimeletwa na kuthibitisha matumizi hayo hivyo HOJA HII IMEFUNGWA.</p>

NA	MAELEZO YA HOJA	USHAURI WA MKAGUZI	MAJIBU YA OFISI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA MKAGUZI BAADA YA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI
	na mwongozo wa uhasibu wa mwaka 2009 kifungu namba 23(1) ambacho kinaagiza kwamba matumizi yote au kiasi chote kilicholipwa au kutumika katika kipindi Fulani lazima kioneshwe kama kilivyo kulingana na kumbukumbu za maingizo.		kamili utaletwa kwa wakaguzi kwa ajili ya majadiliano na uhakiki.		
8	<p><b>Malipo ya Tshs 15, 840,000 Yalifanyika Bila Kwanza Kupokelewa Vipuri vya Greda la Halmashauri.</b></p> <p>Baada ya kupitia nyaraka za manunuzi tulibaini malipo ya kiasi cha Tshs 15,840,000 yaliyofanyika kulipia vipuri vya greda la halmashauri. Hata hivyo vipuli hivyo havikupokelewa hadi sasa.</p> <p>Aidha kitendo cha kutokabidhiwa vipuli vilivyolipwa gharama ni kinyume na Mwongozo wa uhasibu wa mwaka 2009 kifungu 71 (1) (b) ambacho kinaelekeza malipo ya manunuzi.</p>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kuwa vipuri hivi vinaletwa mara moja.</li> <li>2. Maelezo ya kuchelewesha vipuli hivyo yatolewe.</li> </ol>	Hakuna majibu mpaka tarehe 18.01.2017	Mkaguzi afuatilie kwa kina mchakato wa malipo ya Sh. 15,840,000 kuanzia dokezo hadi hundi ili wahusika wajulikane kuanzia mwaandaaji wa vocha hadi watia saini.	Hadi kufikia tarehe 27/02/2017 vipuri vyenye gharama ya shs. 10,290,000 bado havijapokelewa na kitengo cha manunuzi. Tunashauri Mkurugenzi achukue hatua stahiki kwa Muuzaji.